

# TAWHIDI KHALISI

KIMEANDIKWA NA
MUHAMMAD IBN ,ABDUL WAHHAB

KIMEHARIRIWA NA
ABU ANAS AL HUSAIN IBN 'UMAR MAZUZY

## كشف الشبهات في التوحيد

للإمام المجدد شيخ الإسلام : محمد بن عبد الوهاب رحمه الله
باللغة السواحلية

المكتب التعاوني للدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالمعذر وأم الحمام

# TAWHIDI KHALISI

# كشف الشبهات في التوحيد

KIMEANDIKWA NA
MUHAMMAD IBN 'ABDUL WAHHAB

KIMEHARIRIWA NA
ABU ANAS AL HUSAIN IBN 'UMAR MAZUZY

KIMEFASIRIWA NA
SULAYMAN A.S. SHAQSSY

# DIBAJI

Tunamshukuru Allah kwa kumwezesha ndugu yetu Sulayman Shaqssy kukitafsiri kitabu hiki cha Sheikh Muhammad ibn Abdul Wahhab kilichoweka wazi mengi katika maisha ya Muislamu. Kwani Tawhidi ni msingi wa kwanza unaowajibika uwekwe sawa na Muislamu; akitofanya hivyo atakosa hadhi yake hapa duniani, na kesho Akhera atapita patupu.

Mwisho nawashukuru Al-Muntada-Al-Islam kwa kugharamia uchapishaji wa kitabu hiki.

Pasina kumsahau kila aliyeshiriki kukifanya kitabu hiki kuweza kusomwa na Waislamu.

**Abu Hamza**
5/6/96

## UTANGULIZI II

Hakika shukrani zote za dhati zamstahikia Allah. Ambaye twamtaka msaada na msamaha. Na twajilinda kwa Allah kutokana na shari za nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Aongozwaye na Allah hana wa kumpoteza, na Allah akimwachia kupotea, basi hana wa kumwongoza. Na twashuhudia kuwa hapana Mola apasaye juabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, peke yake bila mshirika, na kwashuhudia pia kuwa Muhammad ni mja na Mtume Wake.

Amma ba'd:

Namshukuru kwa dhati Allah Ambaye ameniwafikia kuandika maelezo na fafanuzi hizi juu ya kitabu cha Marehemu Al-Imam Al-Mujaddid, Shaikhul-Isam Muhammad ibn 'Abdul-Wahhab kiitwacho: *"Khashfush-Shubuhat fit-Tawhid.* Na ni kitabu chenye faida kubwa, juu ya udogo wake, kwa vile chenyewe chafedhehi ghururi za watu wa upotofu. Nacho chazivunja zile zichukuliwazo na wanaotawassali na makaburi kuwa ni hoja nzito, ambapo hakika ni upotevu mtupu waliofundishwa na mashetani wao, basi wakapotea na wakawapoteza wengi; na hata sasa wanapotea njia iliyo sawa.

Basi kwa sababu hiyo akasimama Marehemu Shaikhul-Islam, vile itakikanavyo kusimama wanazuoni katika kubainisha haki na kuinusuru, na kuifedhehi batili na kuirudi—aliyafanya hayo katika kitabu au Risalah yake hii tukufu.

Nasi twamwomba Allah awaongoze hao ambao itikadi zao kwa Allah (s.w.) zimedhoofu na badili yake zikashamili imani zao kwa watakatifu wao waliomo makaburini na waliohai pamoja na mashekhe wa Tasawwuf na Tariqah.

Nami siamini kuwa watu kama hao wanajua uwongofu na Tawhidi, au kwa makusudi wameugeuka kwa inadi na kibri, hasha siamini hayo. Hakika ya mambo ni kwamba wao wafanya hivyo kwa kutojua 'aqidah khalisi na safi ya Kiislamu, ambayo ndiyo 'aqidah ya *Ahlis-Sunnah wal-Jama'ah.* Ni matarajio yangu kuwa wataisoma Risalah hii tukufu kwa lengo la kustafidi na kuuona uongofu, kwani Haki yastahiki zaidi kufuatwa, na Allah ndiye tumtegemeaye.

Na shirki ihadhari kwani shirki idhahiri,

Nayo yahiliki wala haina msamaha.
Ni kujichukulia mshirika na Rahmani,
Yeyote Awaye: jiwe au miongoni mwa watu.
Humwomba akatarajia kumjibu na humcha,
Naye kumpenda kama upendo wa Dayyani.

Basi fanya haraka ewe ndugu yangu—na Allah atuongoze sote: mimi na wewe—katika Njia iliyonyoka—fanya haraka kutubia madamu bado kuna uwezekano, kwani atubiaye kabla roho yake haijafika kooni Allah humkubalia toba yake,[1] na pia atubiaye kabla jua halijaanza kuchomoza kutoka magharibi Allah atamkubalia toba yake[2]. Na ambaye ilipatikana kwake sehemu ndogo katika ibada ya makaburi, basi asikate tamaa na rehema ya Allah, kwani toba huyafuta yale yote yaliyo kabla yake; na Allah amesema:

قُلْ يَٰعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ أَسْرَفُوا۟ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا۟ مِن رَّحْمَةِ ٱللَّهِ ۚ إِنَّ
ٱللَّهَ يَغْفِرُ ٱلذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ

*"Sema: 'Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Allah; bila shaka Allah husamehe dhambi zote; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu'."*

## Kazi yangu katika Risalah hii

| | |
|---|---|
| Kwanza: | Nimetaja nambari za aya takatifu za Qur'ani. |
| Pili: | Nimetaja zipatikanako hadithi na kukhusu maudhui zake. |
| Tatu: | Nimeashiria dalili alizozitaja Al-Imam kutoka katika Sirah ya Mtume (s.a.w.) na nikaashiria zipatikanako katika vitabu vya Sunnah na vyenginevyo. |
| Nne: | Nimeiongeza ziada muhimu niliyoikuta katika nuskha ya Al-Allamah Muhibbud-Din Al-Khatib, ziada ambayo haipatikani katika nuskha zote zengine hata ile iliyohaririwa na Al-'Allamah |

---

1. Ishara kwa hadithi ya 'Abdullahi ibn 'Umar kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Allah huikubali toba ya mja madamu hajaanza kukoroma kwa *sakaratil-maut.*" *(Tirmidhi)*

2. Ishara kwa hadithi ya Abu Hurairah (r.a.) kuwa Mtume (s.a.w.) amesema: "Atakayetubu kabla jua halijachomoza kutoka magharibi, Allah atamkubalia toba yake. *(Muslim)*

Ibn Mani' na niliyoichukulia kuwa ndiyo iliyokuwa msingi wa ile nuskha iliyoandikwa kwa khati ya mkono na ambayo imehifadhiwa katika khazina ya vitabu ya *Darul-Matba'ah As-Salafiyyah* ya Cairo.

Tano: Nimekitungia faharisi tano:

— Faharisi ya Aya za Qur'ani.
— Faharis ya Hadithi za Mtume (s.a.w.).
— Faharis ya vitabu vya marejeo.
— Faharisi ya yaliyomo na faida mbalimbali.

Na mwishowe namshukuru Sheikh Safar ibn 'Abdur-Rahman Al-Hawaly na Sheikh Wasiyyul-Lah Muhammad 'Abbas kwa nasaha, irshadi na maelekezo yao na kuipitia Risalah hii nzuri. Basi Allah awajazi kheri na thawabu nyingi.

Hii ni juhudi ya mwenye taqsiri na upungufu, nasi twamwomba kabuli Allah na Aniandikie thawabu Zake kwa ukarimu na ihsani Yake, na Anighufirie na wazazi wangu wawili na Waislamu wote—Amin!

Abu Anas Al-Husain ibn 'Umar Mazuzy.

# BISMILLAHIR-RAHMANIR-RAHIM

## TAWHIDI KHALISI

Fahamu ewe ndugu yangu kuwa Tawhidi ni kumpwekesha Allah (s.w.) kwa ibada, nayo ndio msingi wa Dini ya Mitume wote wa Allah ambayo kwayo Aliwatuma kwa waja Wake. Mtume au Rasuli wa kwanza alikuwa Nuh (a.s.)[1] ambaye alimtuma Allah (s.w.) kwa watu wake pale walipochupa mipaka katika kuwatukuza waja wema wa Allah (s.w.): Wadd, Suwa', Yaghuth, Ya'uq na Nasr[2]. Na wa mwisho miongoni mwa Mitume ni Muhammad (s.a.w.) naye ndiye aliyevunja sanamu za hao waja wema. Allah (s.w.) alimtuma kwa watu ili wafanye ibada, wahiji, watoe sadaka na wamtaje Allah (s.w.) kwa wingi, lakini wao wanafanya baadhi ya viumbe kuwa wasita baina yao na Allah (s.w.), wakisema: 'Hawa twawahitajia ili kujikurubisha kwa Allah (s.w.)', na twahitaji watushufaie Kwake, kama Malaika watukufu, 'Isa ibn Maryam na wengine miongoni mwa waja wema na Allah (s.w.). Hapo Allah (s.w.) akamtuma Muhammad (s.a.w.) ili awajadidishie Dini ya baba yao, Ibrahim (a.s.), na awaambie kuwa kujikurubisha kwa aina hiyo na itikadi namna hiyo ni haki ya Allah (s.w.) peke yake, wala haisilihi sehemu yake yoyote kwa Malaika mtukufu wala Nabii 'Isa, achilia mbali viumbe wengine. Na kwa hakika hawa mushriki wanakiri na kushuhudia kuwa Allah (s.w.) tu ndiye Muumba na kwamba hamna anayeruzuku isipokuwa Yeye, wala ahuishaye ila Yeye wala afishaye ila Yeye; wala hapana apelekaye mambo ila Yeye, na kwamba mbingu zote saba na ardhi zote na vyote vilivyomo ndani yake ni viumbe Vyake na vimo chini ya mamlaka na madaraka Yake.

---

1. Haya ni kwa mujibu wa hadithi iliyosimuliwa na Anas (r.a.) iliyopo katika *Fat-hul-Bary* 11/325 nambari 6365, katika hadithi ya shafa'ah: "... 'Na atasema: Nendeni kwa Nuh ambaye ni Risuli wa kwanza aliyemtuma Allah'..."

Amesema Al-Hafidh Ibn Hajar: "Na jambo hili kuwa Nuh (a.s.) ndio Rasuli wa mwanzo limeleta mushkili... na jawabu lake limeshatangulia katika sherehe ya hadithi ya Jabir katika kitabu: 'At-Tayammum' 1/520.

Pia angalia Kitabu: *'Bad' al-Wahy'* pia hadithi za Abu Hurairah (r.a.) katika *Sahih Muslim* katika hadithi ya Shafa'ah: "...Basi watamwendea Nuh (a.s.) na kumwambia: 'Ewe Nuh! Wewe ndiye Rasuli wa mwanzo kutumwa ardhini..." nambari 92 *Mukhtasar Al-Mundhiry* kilichorejelewa na Al-Albany. Na pia imenakiliwa na *At-Tirmidhiry* nambari 1982 katika *Sahih As-Sunan cha Al-Albany.* Na Ibn Abi 'Asiam katika Kitabus-Sunnah, nambari 811 kilichorejelewa na Al-Albany uk. 366.

Na kama unataka uthibitisho kuwa hao mushriki alowapiga vita Mtume (s.a.w.) kuwa wakiamini namna hiyo tuliyoitaja, basi soma kauli Yake (s.w.):

*Sema: "Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua) na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)? Au ni nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na nani atengezaye mambo yote? Watasema: "Ni Allah". Basi sema: "Je, hamuogopi? (Mnawaabudu wengine pamoja Naye)!"* (10:31)

Na: ﴿قُل لِّمَنِ الْأَرْضُ وَمَن فِيهَا إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ.
قُلْ مَن رَّبُّ السَّمٰوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ. سَيَقُولُونَ لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ.
قُلْ مَن بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ
قُلْ فَأَنَّىٰ تُسْحَرُونَ﴾

*Sema: "Ni ya nani ardhi na vilivyomo ndani yake; kama nyinyi mnajua kitu?" Watasema: "Ni vya Allah." Sema: Basi je, hamukumbuki (kuwa Allah ni Muweza)?" Sema: "Ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa 'Arshi kuu?" Watasema: "Ni vya Allah." Sema: "Basi je, hamumuogopi?" Sema: "Ni nani mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, Naye ndiye Alindaye, na hakilindwi (chochote) kinyume Naye, kama mnajua (jambo nambieni hili)." Watasema: "(Uwezo huo) ni wa Allah." Sema: "Basi vipi mnadanganywa (na shetani mkadanganyika)?"* (23:84-89)

---

Na pia umeinakili Sheikh wetu katika *As-Sahihah* 3/280 nambari 1289, naye akasema kuwa ile hadithi kuwa "Nabii wa kwanza kutumwa ni Nuh" nayo ilisimuliwa na Anas katika Sahih al-Jami' 2585; pia angalia hadithi katika *Al-'Aqidah at-Tahawiyyah* uk. 254.

2. Baada ya kuwa watu walikuwa Ummah mmoja juu ya Tawhidi ukaja upotofu; na upotofu wa kwanza kabisa ulikuwa ni kuchapa mipaka katika kuwatukuza waja wema, na kuwanyanyua hadi daraja na miungu iabudiwayo. Katika *Sahih al-Bukhari* 8/535 na al-fat-h amesimulia Ibn 'Abbas katika kuifasiri kwake kauli ya Allah:

Na ambao waliwaambia (wafuasi wao): *'Msiache miungu yenu, wala msiwaache Waddi wala Suwa'a wala Yaghutha wala Ya'uqa wala Nasra.'* (71:23)

Akasema (r.a.): "Haya ni majina ya waja wema miongoni mwa watu wa Nuh; walipofariki, shetani aliwashawishi wasimamishe masanamu katika makazi yao kisha wayaite masanamu hayo kwa majina yao, nao wakafanya hayo. Basi hayakuabudiwa mpaka walipofariki wenyewe."

Pia angalia sherehe ya hadithi hiyo katika *Fat-hul Bary* na kitabu cha *Al-'Aqidah fil-Lah, uk.* 247 cha Ustadh 'Umar Sulayman Al-Ashqar.

Na kuna aya nyingi zingine kama hizo. Basi ikishathibiti kuwa wao wanakiri jambo hili la *Tawhidir-Rububiyyah* na kwamba hilo pekee halikuwaingiza katika Tawhidi aliyowalingania Mtume (s.a.w.), hapo utafahamu kuwa Tawhidi waliokanusha ni Tawhidi ya 'ibada ambayo washirikina wanaiita *Al-I'tiqad;* kama ambavyo walikuwa wakimwomba Allah usiku na mchana kisha baadhi yao wakiwaomba Malaika kwa ajili ya mafanikio na ukuruba wao kwa Allah. ili wawashufaie, au wakimwomba mtu mwema kama vile Allat au Nabii kama 'Isa (a.s.), hapo utafahamu kuwa Mtume (s.a.w.) alipigana nao kwa sababu ya shirki hii na akawalingania katika kukhalisisha 'ibada kwa ajili ya Allah peke yake, kama asemavyo Allah (s.w.):

قال تعالى: ﴿وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا﴾ [سورة الجن، الآية: ١٨]

*Na kwa hakika misikiti (yote) ni ya Allah, basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah.* (72:18)

Na: قال تعالى: ﴿لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُمْ بِشَيْءٍ﴾ [سورة الرعد، الآية: ١٤].

*Kwake (Allah) ndiyo yako (maitikio ya) maombi ya haki. Na wale wanaowaomba badala Yake (Allah) hawawajibu chochote.* (13:14)

Hapo utakuwa umehakikisha kwamba Mtume (s.a.w.) alipigana nao ili du'a zote zielekezwe kwa Allah (s.w.), nadhiri zote zifanywe kwa ajili ya Allah na kujikinga kuwe kwa Allah; na aina zote za 'ibada ziwe kwa ajili ya Allah tu peke yake, utafahamu kuwa kuikiri kwao *Tawhidir-Rububiyyah* hakukuwaingiza katika Uislamu. Na kuwaomba kwao Malaika, Manabii au mawalii wakitaka shufa'a zao na kujikurubisha kwa kuwatumia hao kama wasita, ndiko kulikohalalisha damu na mali zao. Hapo ndipo utakapoijua Tawhidi waliolingania Mitume (a.s.) na wakaikataa washirikina; na Tawhidi hiyo ndiyo inayomaanisha kauli yako: *'La ilaha illal-Lah',* yaani: "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah." Basi Mola kwao wao ambaye kwa ajili ya malengo kama haya, awe ni Malaika, Nabii, walii, mti, kaburi au jini hawamaanishi kuwa mola huyo ndiye Muumba, Mruzuku na Mpelekaji wa mambo—kwani wao wanajua kuwa hayo nivya Allah kama nilivyoeleza awali

kwa aya za Qur'ani. Kwa Mola, wao wanamaanisha kile wanachomaanisha washirikina wa zama zetu hii kwa jina la Sayyid au Bwana; ndipo akawajia Mtume (s.a.w.) akiwalingania katika neno la Tawhidi: *La ilaha illal-Lah,* na muradi wa neno hili ni maana yake wala si tamshi lake.

Na makafiri majahili wajua kuwa muradi wa Mtume (s.a.w.) kwa neno hili ni: Kumpwekesha Allah (s.w.) kwa kumtegemea Yeye tu peke yake kwa mambo yote na kuwakanusha na kujitenga na wale wote waabudiwao kinyume na Allah. Kwani Mtume (s.a.w.) aliwaambia: "Semeni: *"La ilaha illal-Lah';* wao walisema:

﴿أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ﴾ [سورة ص، الآية: ٥]

*Oh: Amewafanya miungu (wote) kuwa Mungu Mmoja tu! Bila shaka hili ni jambo la ajabu.* (38:5)

Basi ukishafahamu kuwa hata majahili miongoni mwa makafiri walijua hilo, la kushangaza ni kuwa vipi wanaojidai Uislamu washindwe kujua tafsiri ya neno hili ambayo makafiri majahili wameijua? Bali mtu kama huyo hudhani kuwa lengo ni kulitamka tu bila kuiitakidi kwa moyo maana yake. Na mwerevu miongoni mwao hudhani kuwa maana yake ni: "Haumbi wala haruzuku wala hapeleki mambo ila Allah." Basi hana kheri yule ambaye hata majahili, makafiri waijua zaidi kuliko yeye maana ya *La ilaha illal-Lah.* Na ukishayajua vema niliyokuambia, na ukaijua shirki ya kumshirikisha Allah (s.w.), ambayo Allah ameizungumizia hivi:

﴿إِنَّ اللهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ﴾ [سورة النساء، الآية: ٤٨]

*Hakika Allah hasamehi kushirikishwa; na Husamehe yasiyokuwa haya kwa Amtakaye.* (4:48); na ukaijua Dini ya Allah (s.w.) ambayo kwayo Alituma Mitume (a.s.) toka wa kwanza mpaka wa mwisho, Dini ambayo Allah hakubali kwa mtu yeyote isipokuwa Dini hiyo, kisha ukajua jinsi watu wengi walivyo wajinga na jambo hilo; hayo yote yatakufindisha faida mbili:

Kwanza: Kuifurahia fadhla ya Allah na rehema Yake, kama alivyosema Allah (s.w.):

قال تعالى: ﴿قُلْ بِفضلِ الله وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ﴾

[سورة يونس، الآية: ٥٨].

*Sema: "Kwa fadhla za Allah na kwa rehema Yake, basi na wafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko wanayoyakusanya."* (10:58)

Pili: Pia utafaidika kutokana na khofu kubwa, kwani utakapofahamu kuwa mtu hukufuru kwa neno tu alitoalo ulimini mwake, na pengine hulitamka na hali yeye ni mjinga asiyejua hakika ya mambo, na juu ya hivyo udhuru wake wa ujinga usikubaliwe*, au pengine alitamke huku akidhani kuwa neno hilo litamkurubisha kwa Allah kama wadhanivyo washirikina; na khasa ukiiona kauli ya Allah kukhusu walivyosema Wayahudi kumwambia Musa (a.s.):

﴿اجعَل لنا إلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ﴾ [سورة الأعراف، الآية: ١٣٨].

*Ewe Musa! Tufanyie waungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu.* (7:138)

Basi hapo ndipo khofu yako huzidi na kujitahidi kukhalisisha Tawhidi yako mpaka ikuepushe na mambo kama haya.

Tena ujue, Allah hakumtuma Nabii yeyote na Tawhidi kama hii isipokuwa huwa na maadui kama alivyosema Mwenyewe Allah (s.w.):

﴿وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيَاطِينَ الإِنسِ وَالجِنِ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ القَولِ غُرُورًا﴾ [سورة الأنعام، الآية: ١١٢]

*Na namna hii Tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na katika majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya.* (6:112)

Na huenda hao maadui wa Tawhidi wakawa na elimu nyingi na vitabu na hoja kama Alivyosema (s.w.):

قال تعالى: ﴿فَلَمَّا جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَرِحُوا بِمَا عِنْدَهُم مِّنَ الْعِلْمِ﴾

[سورة غافر، الآية: ٨٣].

*Basi walipowajia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi walifurahia elimu waliyokuwa nayo.* (40:83)

Ukishajua hayo na ukajua pia kuwa Njia iongozayo kwa Allah (s.w.) haina budi iwe na maadui wameikalia, nao yawezekana kuwa ni watu mafasihi, wenye ujuzi na hoja, basi wajibu wako ujue katika Dini ya Allah yale ambayo yatakuwa ni silaha yako ya kuwapiga vita mashetani hao ambao kiongozi wao alimwambia Mola wako Mtukufu:

﴿لَأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ ثُمَّ لَآتِيَنَّهُم مِّن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَن شَمَائِلِهِمْ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ﴾ [سورة الأعراف، الآيات: ١٦، ١٧].

*...Basi nitawakalia (waja Wako) katika Njia Yako iliyonyoka (ili niwapoteze). Kisha nitawafikia kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao na kushotoni kwao; na wengi katika wao Hutawakuta ni wenye kushukuru.* (7:16-17)

Lakini ukimwelekea Allah (s.w.) na ukazizingatia hoja na mafafanuzi Yake basi huna cha kuogopa wala cha kuhuzunikia kwani:

﴿إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا﴾ [سورة النساء،

*Hakika hila za shetani ni dhaifu.* (4:76)

Na mtu wa kawaida tu katika Tawhidi huwashinda elfu miongoni mwa wanazuoni wa hao washirikina kama alivyosema (s.w.):

﴿وَإِنَّ جُندَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ﴾ [سورة الصافات، الآية: ١٧٣]

*Na jeshi Letu ndilo litakaloshinda.* (37:173)

Basi askari wa Allah ndio washindao kwa hoja na ulimi, na pia ndio washindao kwa panga na mikuki. Lakini khofu ni juu ya Muwahhidi ambaye aingia katika Njia hiyo bila silaha, hali ya kuwa Allah ametufadhili kwa Kitabu Chake ambacho Amekifanya chenye kufafanua kila jambo, nacho ni Uongozi, rehema na khabari njema kwa Waislamu.

Kwa hiyo, mtu wa batili haji na hoja ila katika Qur'ani kuna ya kuibatilisha na kubainisha ubatili wake kama Alivyosema (s.w.):

---

*Angalia Risalah yangu: Mazaliq fy Tariqi Talib al-'Ila, tazama nambari 10.

قال تعالى: ﴿وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا﴾ [سورة الفرقان، الآية: ٣٣].

*Wala hawatakuletea mfano (wowote), ila Tutakuletea (Aya iliyo ya) haki (kujibu mfano huo) na (kukuletea) tafsiri iliyo bora.* (25:33)

Wamesema baadhi ya wafasiri wa Qur'ani kuwa aya hii yakhusu kila hoja wailetayo watu wa batili mpaka Siku ya Qiyama* nami nakutajia baadhi ya mambo aliyoyataja Allah katika Kitabu Chake kama jawabu kwa kila majidai ya washirikina katika zama zetu hizi. Nao wamejibiwa kwa ufupi na kwa tafsili.

Mfano wa jibu kwa ufupi ni ile amri kuu na faida kubwa kwa mwenye kuitambua na kuielewa, nayo ni kauli Yake (s.w.):

﴿هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ﴾ [سورة آل عمران، الآية: ٧].

*Yeye ndiye Aliyekuteremshia Kitabu (hiki Qur'ani). Ndani yake zimo Aya Muhkam (nyepesi kufahamika) ambazo ndizo msingi (asili wa Kitabu (hiki). Na ziko nyengine Mutashabihat (zinababaisha, kama khabari za Akhera, za Peponi na Mtoni na mengineyo ambayo yamekhusika na roho). Wale ambao nyoyoni mwao mna upotofu wanafuata zile zinazobabaisha kwa kutaka kujua hakika yake vipi, na hakuna ajuaye hakika yake vipi; ila Mwenyezi Mungu.* (3:7)

Na imethibiti kuwa Mtume (s.a.w.) amesema:

«إذا رأيتم الذين يتبعون ما تشابه، فأولئك الذين سمّى الله فاحذروهم»(1).

"Mkiwaona wale wanaofuata zile aya zinazobabaisha, hao ndio wale aliowataja Allah (s.w.), basi tahadharini nao." *(Bukhari, Muslim)*

---

*Nawanasihi wasomaji wasome kitabu muhimu kiitwacho: Tahkim an-nadhir bima Jara minal-Ikhtilafi baina Ummat Abil-Qasim (s.a.w.), cha Salih bin Ahmad; Jami'atul-Islamiyyah, Madinatul-Munawwarah.

Na mfano wa hayo ni kama vile walivyosema washirikina:

﴿أَلاَ إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللهِ لاَ خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلاَ هُمْ يَحْزَنُونَ﴾ [سورة يونس، الآية: ٦٢].

*Sikilizeni! Vipenzi vya Allah hawatakuwa na khofu (Siku ya Qiyama) wala hawatahuzunika.* (10:62)

Au kwa mfano atoe dalili kuwa shafa'ah ni haki; au kuwa Manabii wana jaha kwa Allah, au ataje baadhi ya maneno ya Mtume (s.a.w.) kama ni hoja ya kuipigania batili yake—nawe hufahamu maana na lengo la maneno yake, basi mjibu kuwa: Allah ametaja katika Kitabu Chake kwamba wale wenye maradhi nyoyoni huziacha aya *Muhkam* na kuzifuata ambazo ni *Mutashabih*. Na kumbuka yale niliyokutajia hapo kabla kuwa washirikina wanakiri Uungu wa Allah nao ni makafiri kwa kujing'ang'aniza kwa Malaika, Manabii, Mawalii wakisema:

﴿هؤلاء شفعاؤنا عند الله﴾ [سورة يونس، الآية: ١٨].

*Hao (waungu wadogo washirika Wake tunaowaabudu) ndio waombezi wetu mbele ya Allah.* (10:18)

Na ewe mushrik, hili ni jambo bayana, hakuna awezaye kubadilisha maana yake. Au hayo uliyonitajia katika Qur'ani au maneno ya Mtume (s.a.w.) mimi sijua maana yake, lakini naitakidi kuwa maneno ya Allah hayapingani; na maneno ya Mtume (s.a.w.) hayaendi kinyume na Qur'ani. Hili ni jawabu zuri maridhawa[1]; lakini halifahamu ila mwenye kuwafikiwa na Allah, basi usilidharau, kwani hakika yake ni kama Alivyosema, (s.w.):

﴿وَمَا يلَقَّاهَا إِلاَّ الذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلَقَّاهَا إِلاَّ ذو حَظٍّ عظيم﴾ [سورة فصّلت، الآية: ٣٥].

*Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Allah).* (41:35)

Ama jawabu kwa urefu, basi kwanza utafahamu kuwa maadui wa Allah wana

1. Kwa vile watu wa haki waifahamu Qur'ani na Sunnah kwa fahamu ya Masahaba na waliowafuatia, ndio ikawa ufahamu wao haupotezi, kwa uwezo wa Allah.

aina nyingi za upinzani dhidi ya Dini ya Mitume wa Allah; pinzai ambazo kwazo wanawazuilia watu na Dini ya Allah, miongoni mwake ni majidai yao: Sisi hatumshirikishi Allah kwa chochote, bali twashuhudia kwamba hakuna anayeruzuku, anayeleta madhara na nafuu ila Allah peke yake, Ambaye hana mshirika; na kwamba Muhammad (s.a.w.) haimilikii nafsi yake madhara wala manufaa.[2] Licha ya Abdul-Qadir[3] au wengine, lakini mimi ni mwenye dhambi na waja wema wa Allah wana jaha Kwake; nami namwomba Allah kupitia kwao. Basi mjibu kwa yale majibu yaliyotangulia, kwamba wale alowapiga vita Mtume (s.a.w.) wanayakiri hayo uloyataja, na pia wanakiri kuwa masanamu yao hayana uwezo wa kufanya lolote, bali wao walitaka kwa hayo masanamu jaha na shafa'ah.

Na msomee aloyataja Allah katika Kitabu Chake na mfafanulie.*

---

2. Kwa mujibu wa kauli Yake (s.w.):

﴿قُل لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ وَلَوْ كُنتُ أَعْلَمُ الْغَيْبَ لَاسْتَكْثَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ السُّوءُ إِنْ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾ [سورة الأعراف، الآية ١٨٨].

*Sema: "Sina mamlaka ya kujipa najuu wala ya kujiondoiea madhara ila apendavyo Allah; na lau kama ningelijua ghaibu ningejizidishia mema mengi; wala isingalinigusa dhara; mimi si chochote ila ni Muonyaji na Mtoaji wa khabari njema kwa watu wanaoamini.* (7:188)

Na pia kwa mujibu wa kauli yake Mtume (s.a.w.): "Wala sikufaeni chochote mbele ya; (Qadha) ya Allah." Na pale alipomwambia Bi Fatimah: "Ewe Fatimah binti Muhammad! Niombe ukitakacho katika mali yangu, siwezi kukufaa chochote mbele ya Allah." *(Fat-hul-Bary)*

Na kauli yake (s.a.w.) katika kisa cha kufariki kwa Sahaba atukufu 'Uthman ibn Madh'un: "...Wallahi sijui hali yakuwa mimi ni Mtume wa Allah nitatendewa nini."*(Bukhari)*
*Yaani zile aya zionyeshazo kuwa waabudu masanamu walikuwa wakiyakiri hayo yaliyotajwa, na juu ya hivyo Allah aliwakufurisha na kuibatilisha dini yao, Akamwamrisha Mtume Wake awapige vita vya Jihadi.

3. Sheikh Abu Muhammad, 'Abdul-Qadir bin Abi Salih Al-Jilany, ni mashuhuri mwenye zuhdi na karama, na elimu na maarifa, Sheikh wa Hanabilah, alizaliwa huko Jilani, mwaka 490 H. au 491 H. Alienda Baghdad akiwa bado kijana kujifunza Hadithi kwa Sheikh Abaqlany na Sheikh Ja'far As-Siraj na Abu Bakr bin Sus. Na alijifunza Al-Adabul-Islamy kwa Sheikh Abu Zakariyya Al-Tibrizy na wengineo. Haya yametajwa na Ibn As-Sam'any ambaye pia amesema: Alikubalika kwa watu, nao wakawa na thiqah katika ushikamanaji wake wa Dini na utangamano wake; wakafaidika na maneno na mawaidha yake. Ahlis-Sunnah wakashinda kwa kudhihiri kwake, na hali yake, na kauli yake na karama zake zikawa mashuhuri baina ya watu.

﴿وَإِذْ قَالَ اللهُ يَاعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ اللهِ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ﴾ [سورة المائدة، الآية: ١١٦].

*"Hao wanaowaomba, (wenyewe) wanatafuta ukaribiano na Mola wao; (hata) walio karibu sana miongoni mwao (na Mungu, kama Malaika, wao wanafanya hayo) wanatumai rehema Zake na wanaogopa adhabu Yake. Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuogopwa.* (17:57)

Na wanamwomba 'Isa bin Maryam (s.a.) na mama yake na hali Allah amesema:

*Masihi bin Maryam si chochote ila ni Mtume (tu). (Na) bila shaka Mitume wengi wamepita kabla yake. (Hawajawaona)? Na mama yake ni mwanamke mkweli. (Na) wote wawili walikuwa wakila chakula (na wakenda choo. Basi — gani wanaokula na kwendo choo)? Tazama jinsi Tunavyowabainishia Aya, kisha tazama jinsi wanavyogeuzwa (kuacha haki). Sema: "Je, mnawaabudu badala ya Mwenyezi Mungu (peke-yake)—wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukunufaisheni? Na Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye na Ajuaye.* (5:75:76)

﴿وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلْمَلَائِكَةِ أَهَٰؤُلَاءِ إِيَّاكُمْ كَانُوا يَعْبُدُونَ . قَالُوا سُبْحَانَكَ أَنتَ وَلِيُّنَا مِن دُونِهِم بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ الْجِنَّ أَكْثَرُهُم بِهِم مُّؤْمِنُونَ﴾

*Na (wakumbushe) siku Atakayowakusanya wote, kisha Atawaambia Malaika: "Je, hawa walikuwa wakikuabuduni?" Waseme: "Umeepukana na kila upunguful! Wewe ndiwe Kipenzi chetu, si hao; bali walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao waliwaamini hao (majini)."* (34:40-41)

Na kauli Yake (s.w.): ﴿قَالَ اللهُ يَاعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ اللهِ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ﴾

*Na (kumbukeni) Allah atakaposema: "Ewe 'Isa bin Maryam! Je, wewe uliwaambia watu: 'Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa waungu badala ya*

---

Amesema Abu Sa'd As-Sam'any na Al-Hafidh 'Abdul-Ghaniy kuwa Sheikh 'Abdul-Qadir Jilany alikuwa kiongozi wa watu wa zama zake na pia Sheikh wa Masheikh wa zama zake. Alifariki mwaka 561 H. (Angalia: *Taj Al-Mukallal* uk. 166 cha *Abu At-Tayyid Al-Bukhary Al-Qanujy*. Pia angalia: Sayr A'lam An-Nubala, 20/439 cha Imam Adh-Dhahaby)

*Allah?" Aseme (Nabii 'Isa): "Wewe Umetakasika na kuwa na mshirika. Hainijuzii mimi kusema ambayo si haki yangu (kuyasema, kwa kuwa ni ya uwongo). Kama ningelisema bila shaka Ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajuui yaliyo nafsini Mwako; hakika Wewe ndiye Ujuaye mambo ya ghaibu."* (5:116)

Mimi ni mwenye dhambi na waja wema wana jaha kwa Mwenyezi Mungu, nami naomba kwa Mwenye Mungu kupitia kwao; basi mpe jibu lililotangulia, nalo ni kwamba wale amabao aliwapiga vita Mtume (s.a.w.) pia walikiri hayo hayo uliyoyataja, na walikiri kuwa masanamu yao hayawezi kufanya lolote; bali wao wanatafuta jaha na shafa'ah kupitia kwao.

Basi hapo umwambie: Je, umefahamu kuwa Allah amewakufurisha wanaoyakusudia masanamu kwa du'a na maombi, na Amewakufurisha pia wanaowaomba waja wema; naye Mtume (s.a.w.) akawapiga vita? Akisema: "Makafiri wanawaomba wao, nami nashuhudia kuwa Allah ndiye Mwenye kufaa na Mwenye kudhuru na Mwenye kuendesha mambo; mimi siombi chochote ila kutoka Kwake, na waka wema hawana lao katika mambo haya, ila mimi nawakusudia wao nikitarajia shufa'ah yao kutoka kwa Allah. Basi jawabu ni kwamba kauli hii ni sawa na kauli ya makafiri. Na hapo msomee kauli Yake (s.w.):

فالجواب أن هذا قول الكفار سواء بسواء، واقرأ عليه قوله تعالى: ﴿والذين اتخذوا من دونه أولياء ما نعبدهم إلا ليقربونا إلى الله زلفى﴾ [سورة الزمر، الآية: ٣]. وقوله تعالى:

*Lakini wale wanaowafanya wengine kuwa waungu badala Yake (husema:) 'Sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na Allah.'* (39:3)

Na kauli Yake (s.w.): ﴿ويقولون هؤلاء شفعاؤنا عند الله﴾ [سورة يونس، الآية: ١٨].

*Na wanasema: 'Hao (waungu wadogo washirika Wake tunaowaabudu) ndio waombezi wetu mbele ya Allah.'* (10:18)

Na ufahamu kuwa aina tatu[1] hizi za kuchanganikiwa ndio majidai makubwa kwao. Lakini ukijua kuwa yamefafanuliwa vema na Allah katika Kitabu Chake, nawe ukayafahamu vilivyo basi utatambua ni sahali mno kuyarudi mambo hayo.

Akisema: "Mimi simwabudu ila Allah, na kwa hivyo, kuwaelekea wao kwa du'a si 'ibada." Wewe mwambie: "Je, wewe unakiri kuwa Allah amekuwajibishia kukhalisisha 'ibada kwa ajili Yake tu nayo ni haki Yake juu yako?" Na ikiwa hajui 'ibada na aina zake, basi mbainishie kwa kauli Yake (s.w.):

﴿ادعوا ربكم تضرعًا وخفية إنه لا يحب المعتدين﴾ [سورة الأعراف، الآية: ٥٥].

*Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri (kwa sauti ndogo bila ya kelele). Yeye (Allah) hawapendi wapitao mipaka.* (7:55)

Ukishamjulisha hayo, muulize: "Je, umeshafahamu kuwa hii ndio 'ibada ya Allah?" Bila shaka atasema: "Ndio, na dua ndio ubongo wa 'ibada." Hapo mwambie: "Kama umeshakiri kuwa hiyo ni 'ibada.[1], nawe ukamwomba Allah usiku na mchana kwa khofu na matarajio, kisha kwa haja hiyo hiyo ukamwomba Nabii au mwengine, je, utakuwa umeshirikisha mwengine katika 'ibada ya Allah?" Bila shaka atasema: "Naam." Basi mwambie: "Ukiitekeleza amri ya Allah iliyomo katika kauli Yake:

بقول الله تعالى: ﴿فصل لربك وانحر﴾ [سورة الكوثر، الآية: ٢]

*Basi sali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako).* (108:2)

Kisha ukamtii Allah na ukachinja kwa ajili Yake, si utakuwa umefanya 'ibada?" Bila shaka atasema: "Naam." Mwambie: Je, ukichinja kwa ajili ya kiumbe au mwengine, si utakuwa umemshirikisha mwengine katika 'ibada ya Allah (s.w.)? Hapo pia atajibu: "Naam." Mwambie vile vile: Hao washirikina iliyowateremkia Qur'ani, walikuwa wakiabudu malaika, waja wema na Allat, n.k.? Atasema: "Naam." Mwambie: Na hao 'ibada yao kwao si ilikuwa katika du'a na kuchinja na kukimbilia kwao zama za shida? La sivyo, wao walikuwa wakikiri kuwa wao ni waja wa Allah walio chini ya kahari Yake na kwamba Allah ndiye

---

1. Ya kwanza: Kauli yao: "Sisi hatumshirikishi Allah na chochote."
Ya pili: Kauli yao: "Aya kama hizo ziliteremshwa kwa wanaoabudu masanamu."
Ya tatu: Kauli yao: "Makafiri ndio wawaombao hao..." *(Ibn Mani')*

Mwendesha mambo—lakini waliwaomba hao wakakimbilia kwao kwa ajili ya jaha na shufa'ah; na jambo hili ni dhahiri kabisa.

Akisema: "Je, unaikanusha shufa'ah ya Mtume (s.a.w.) na unajitenga nayo?" Sema: Siikanushi wala sijitengi nayo; bali yeye (s.a.w.) ndiye Mwombezi mwenye kukubaliwa[2] na naitarajia sana shufa'ah yake.

Lakini shufa'ah yote ni ya Allah kama alivyosema Yeye Mwenyewe:

﴿قل لله الشفاعة جميعًا﴾ [سورة الزمر، الآية: ٤٤].

*Sema: "Uombezi wote uko katika amri ya Allah."* (39:44)

Wala haiwi hiyo shufa'ah ila baada ya idhini Yake (s.w.) kama alivyotuambia Yeye Mwenyewe:

قال تعالى: ﴿من ذا الذي يشفع عنده إلا بإذنه﴾ [سورة

*Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Allah) bila ya idhini Yake?* (2:255)

Wala hataombewa yeyote ila kwanza aruhusu Allah kuombewa mtu kama huyo, kama alivyosema Allah (s.w.):

قال تعالى: ﴿ومن يبتغ غير الإسلام ديناً فلن يُقبل منه﴾ [سورة آل عمران، الآية: ٨٥].

*Na anayetaka Dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake.* (3:85)

Basi ikiwa shufa'ah yote iko kwa amri ya Allah, wala haitakuwa ila baada ya idhini Yake, wala hataombea Mtume (s.a.w.) na wengine wote kwa ajili ya mtu yeyote mpaka kwanza aruhusu Allah kuombewa mtu kama huyo, wala Allah hataruhusu uombezi ila kwa watu wa Tawhidi—haya yote yanadhihirisha kuwa shufa'ah yote iko kwa umri ya Allah, basi uitake Kwake na useme: "Ewe Allah usinizuiliye uombezi wake Mtume (s.a.w.) na Ukubali uombezi wake

---

1. Ishara kwa hadithi ya Anas (r.a.) katika Sunan At-Tirmidhi (Juz. 9 u.k. 310 At-Tuhfah) kwa isnadi dhaifu, kwani ndani yake mna Ibn Luhay'ah ambaye hana hifdhi nzuri, angalia Al-Mishkat, Na: 2231 na'Dhaif al-Jami', Na: 3003 cha Sh. Al-Albany. Na iliyo Sahihi ni hadithi ya Nu'man ibn Bashir (r.a.): "Ad-Du'au huwal-'ibadah", yaani: "Du'a ndio 'ibada." *(Tirmidhi)*

2. Ishara kwa ile hadithi: "Mimi ndiye Mwombezi wa kwanza Peponi..." *(Muslim)*

kwangu ...", na kama hayo.

Akisema: "Mitume (s.a.w.) amepewa uombezi, nami namwomba kwa lile alilompa Allah." Jawabu ni: Allah amempa uombezi na Akakuzuia wewe usimwombe Mtume (s.a.w.), Aliposema:

قال تعالى: ﴿فلا تدعو مع الله أحدًا﴾ [سورة: الجن، الآية: ١٨].

*Basi msimwabudu (msimwombe) yeyote pamoja na Allah.* (72:18)

Na vile vile shufa'ah wamepewa na wengine zaidi ya Mtume (s.a.w.), ikathibiti basi kuwa malaika nao wataombea, na watoto wadogo[1] nao wataombea, na mawalii nao wataombea[2] basi utasema kuwa kwa vile amewapa uombezi basi nitautafuta kwao? Ukifanya hivyo utakuwa umerudi katika kuwaabudu waja, kama Alivyolitaja hilo Allah katika Kitabu Chake.

Akisema: "Mimi simshirikishi kabisa Allah na chochote, na kukimbilia kwa waja wema si shirki." Mwambie: Kama unakiri kuwa Allah ameharamisha shirki kuliko Alivyoiharamisha zinaa, na unakiri kuwa Allah hasamehe kosa la shirki; basi ni jambo gani hilo aliloliharamisha Allah na kusema kuwa hatalisamee? IKiwa hajui, mwambie: Utajiepusha vipi na shirki na huijui? Vipi Allah aiharimishe kwako na Aseme kuwa Hataisamehe, nawe huijui wala huiulizii? Wafikiri kuwa Allah ataiharimisha kisha Asitubainishie? Akisema: "Shirki ni kuabudu masanamu, nasi hatuabudu masanamu." Mwambie: Kuabudu masanamu kwamaanisha nini? Je, wadhani kuwa wao wanaitakidi kuwa mbao na mawe hayo yanawaumba, yanawaruzuku na kuwaendeshea mambo yao hao wanaoyaomba? Hilo linakidhibishwa na Qur'ani[3]

---

1. Anas (r.a.) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w.) amesema: "Hamna mtu miongoni mwa Waislamu ambaye atafiliwa na watoto wake watatu wadogo kabla ya kubaleghe ila mtu huyo Atamuingiza (Allah) Peponi kwa ajili ya kuwahurumia Kwake." *(Bukhari)*

2. Ishara kwa hadithi marfu' ya Abu Sa'id Al-Khudry (r.a.) kuwa Mtume (s.a.w.) amesema: "Atasema Allah: 'Malaika wameombea, Manabii wameombea na Waumini wameombea na hakubakia ila Allah Ambaye ni Arhamur-Rahimina, hapo Atashika mshiko katika Moto watoke watu ambao hawakufanya kheri kabisa." *(Muslim)*. Angalia: Al-'Aqidah At-Tahawiyyah kilichohaririwa na Al-Albany, uk. 260: Na kitabu: Hukmu Tarikus-Salah cha Al-Albany.

3. Kama alivyosema Allah:

قال الله تعالى: ﴿قل من يرزقكم من السماء والأرض..﴾ [سورة: يونس الآية: ٣١]

*Sema: Ni nani Anayekuruzukuni kutoka mbunguni na katika ardhi ....* (10:31)

Na siri ya mas'ala haya ni kuwa akisema: "Mimi simshirikishi Allah", mwambie: Ni nini kumshirikisha Allah? Hebu nifafanulie. Akisema: "Shirki ni kuabudu masanamu." Muulize: Nini maana ya kuabudu masanamu? Nifasirie. Akisema: "Mimi simwabudu yeyote isipokuwa Allah peke yake." Muulize: Nini maana ya kumwabudu Allah peke yake? Nifafanulie. Kama akifafanua kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'ani, basi hilo ndilo linalotakikana. Na kama hajui, basi atajidaia vipi kitu asichokijua? Na kama akifafanua kinyume na maana khalisi, utawajibika kumbainishia maana ya kumshirikisha Allah na kuabudu masanamu—nalo ndilo walifanyalo zama hizi. Na kumwabudu Allah peke yake ndio jambo wanalotukanushia na kutupigia kelele kama walivyopiga kelele wenzao waliposema:

﴿أجعل الآلهة إلهًا وَاحدًا إنّ هَذَا لشيءٌ عجاب﴾ [سورة ص، الآية: ٥].

*Oh! Amewafanya miungu (wote) kuwa Mungu Mmoja tu! Bila shaka hili ni jambo la ajabu.* (38:5)

Akisema kuwa hao hawakufurishwi kwa sababu ya kuwaomba malaika na Manabii, bali kwa kusema kwao kuwa malaika ni mabinti wa Allah. Nasi hatudai kuwa 'Abdul-Qadir ni mtoto wa Allah, na hivyo hivyo hatuwadaii uungu wengine. Jawabu lake ni: Kumnasibishia Allah mtoto hilo peke yake ni kufuru, kwani Allah Amesema:

قال الله تعالى: ﴿قل هو الله أحد الله الصّمد﴾ [سورة الإخلاص، الآيتان: ١، ٢].

*Sema: 'Yeye ni Allah Mmoja (tu). Allah (tu) ndiye Anayestahiki kukusudiwa (na viumbe Vyake vyote kwa kumwabudu na kumwomba na kumtegemea).'* (112:1-2)

Na Al-Ahad ni Yule asiye na wa kufananishwa Naye. Na As-Samad ni yule Anayekusudiwa kwa kumwomba mahitaji yote*. Basi atakayekanusha haya amekufuru, hata kama hataikanusha Suratul-Ikhlas yote. Na pia Allah amesema:

*Allah hakujipatishia mtoto wala hakuwa pamoja Naye mungu (mwengine)* (23:91)

---

*Ameyasema hayo Al-Hafidh Ibn Kathir katika Tafsiri yake kutoka kwa Ibn A'Abbas, Juz. IV, uk. 609.

Hapa twaona kuwa Allah amezipambanua hizo aina mbili za kufuru na kuifanya kila mojawapo ni kufuru ya aina yake. Na akasema tena Allah:

قال تعالى: ﴿وجعلوا لله شركاء الجنَّ وخلقهم وخرقوا له بنين وبنات بغير علم﴾

[سورة الأنعام، الآية: ١٠٠].

*Na wamemfanyia Allah majini kuwa ni washirika Wake, hali Yeye ndiye Aliyewaumba (si majini). Na wanamsingizia (Allah) kuwa ana watoto wa kiume na wa kike. (Wakasema haya) pasipo kujua.* (6:100)

Hapa pia amezipambanua aina hizo mbali za kufuru.

Na dalili nyengine juu ya jambo hili ni kuwa wale walikufuru kwa kumwomba Allat juu ya kuwa alikuwa ni mtu mwema, nao hawakumchukulia kuwa ni mtoto wa Allah. Na wale waliokufuru kwa kuwaabudu majini hawakuwa-chukulia kama watoto wa Allah. Na kadhalika 'Ulama katika madhehebu zote nne wanasema katika Mlango wa Hukumu ya Murtadi kuwa Muislamu akidai tu kuwa kuna mtoto wa Allah basi huyo ni murtadi; nao wanazipambanua aina mbili hizi za kufuru, na hili ni jambo dhahiri.
Akisema:

قال: ﴿ألَا إنَّ أولياء الله لا خوف عليهم ولا هم يحزنون﴾ [سورة يونس، الآية: ٦٢]

*Sikilizeni! Vipenzi vya Allah hawatakuwa na khofu (Siku ya Qiyama) wala hawatahuzunika.* (10:62)

Mwambie: Hiyo ndio haki, lakini hao hawaabudiwi; nasi hatukutaja ila kuchanganyishwa kwao katika 'ibada pamoja na Allah na kushirikishwa kwao Naye. Bali unawajibika kuwapenda na kuwafuata na kuitambua hishima yao, wala hamna akanushae hishima yao isipokuwa watu wa bid'a na upotofu. Tukumbuke kuwa Dini ya Allah ndiyo mwenendo wa sawa na ndiyo kipambanuzi baina ya haki na batili. Basi ukishafahamu kuwa hii waiitayo washirikina itikadi katika zama zetu hizi, ndiyo shirki khasa iliyosemwa katika Qur'ani na ambayo Mtume (s.a.w.) aliwapigia vita watu, hapo atajua kuwa shirki ya watu wa kale ni nyepesi kuliko shirki ya watu wa zama zetu kwa mambo mawili: Kwanza: Watu wa kale hawakuwa wakiwaomba Malaika,

mawalii na masanamu pamoja na Allah ila katika hali ya neema na utengamano; ama katika shida na misukosuko, basi walikimkhalisia Allah du'a na maombi yote kama atubainishiavyo Allah Mwenyewe:

قال تعالى: ﴿وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَن تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ فَلَمَّا نَجَّاكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ الْإِنسَانُ كَفُورًا﴾ [سورة الإسراء، الآية: ٦٧]

*Na inapokufikieni taabu katika bahari, hupotea wale mnaowaita (waungu hamuwahitaji) isipokuwa Yeye (Allah) tu (Mungu wa haki). Lakini Anapokufikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka. Ama binadamu ni mwingi wa kukanusha (neema za Allah).* (17:67)

Na kauli Yake:

وقوله: ﴿قُلْ أَرَأَيْتَكُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُ اللَّهِ أَوْ أَتَتْكُمُ السَّاعَةُ أَغَيْرَ اللَّهِ تَدْعُونَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ إِن شَاءَ وَتَنسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ﴾ [سورة الأنعام، الآيات: ٤٠، ٤١].

*Sema: 'Niambieni, kama ikikufikieni adhabu ya Allah (ya hapa duniani) au ikikufikieni ile saa (ya kufikiwa na adhabu ya Akhera) je, mtamwita (mtamwomba) asiyekuwa Allah (akuondosheeni) ikiwa nyingi ni wakweli? Bali Yeye ndiye mtakayemwomba, Naye atakuondoleeni mnayomwomba (kukuondosheeni) Akipenda. (Nayo ni yale ya kiduniani si ya Kiakhera), na mtawasahau mnaowashirikisha (na Mungu).* (6:40-41)

Na kauli Yake:

وقوله: ﴿وَإِذَا مَسَّ الْإِنسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ﴾ إلى قوله: ﴿قُلْ تَمَتَّعْ بِكُفْرِكَ قَلِيلًا إِنَّكَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ﴾ [سورة الزمر، الآية: ٨].

*Na taabu inapomfikia mtu humwomba Mola wake, akaelekea Kwake. Kisha*

*akimpa neema kutoka Kwake, husahau yale aliyokuwa akimwitia zamani, na kumfanyia Allah washirika ili apoteze (watu) na Njia Yake (Allah). Sema: (kuwaambia hao makafiri): 'Starehe kwa kufuru yako muda kidogo tu kwani wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.'* (39:8)

Na kauli Yake: وقوله:

﴿وإذا غشيهم موجٌ كالظّلل دعوا الله مخلصين له الدّين﴾

[سورة لقمان، الآية: ٣٢].

*Na mawimbi yanapowafunika kama mawingu, humwomba Allah kwa kumtii kweli kweli.* (31:32)

Basi atakayefahamu kadhia hii ambayo ameiwadhihisha Allah katika Kitabu Chake, nayo ni kuwa washirikina ambao aliwapiga vita Mtume (s.a.w.) walikimwomba Allah na walikiwaomba wengine katika amani na utulivu, lakini katika shida na misukosuko hawakuwa wakimwomba yeyote isipokuwa Allah peke yake, na wakiwasahau mabwana wao; hapo itambainikia tofauti baina ya shirki ya watu wa zama zetu hizi na shirki ya watu wa kale. Lakini ni nani huyo mwenye kujibidiisha kuufahamisha moyo wake hakika ya kadhia hii kwa fahamu sahihi? Wallahul-Musta'an!

Na jambo la pili: Watu wa kale walikuwa wakiwaomba watu pamoja na Allah ambao ni wenye mkuruba kwa Allah; nao ni ama Manabii, mawalii au Malaika; au wakiyaomba mawe au miti: ambavyo ni viumbe vitiifu kwa Allah wala si viasi. Lakini watu wa zama zetu wanawaomba pamoja na Allah mafasiki wa kupindukia miongoni mwa watu, nao ndio wanaowahalalishia maovu kama vile zina, wizi kuacha Salah, n.k.; na mwenye kuwaitakidi waja wema au vile visivyoasi kama mbao au mawe ana nafuu kuliko yule mwenye kuwaitakidi ambao ufasiki na ufisadi wao ni dhahiri shahiri.

Ikibainika kuwa wale alowapiga vita Mtume (s.a.w.) walikuwa na fahamu nzuri zaidi na shirki yao ilikuwa khafifu kidogo kuliko ya hawa wa zama zetu, basi fahamu kuwa hawa wana kuchanganyikiwa wanakokutangaza kama tulivyotaja mwanzoni. Na huko ndio kuchanganyikiwa kwao kukubwa kabisa, basi tega sikio upate jawabu lake. Wao wasema: 'Hao ambao wameshutumiwa katika Qur'ani hawakiri wala hawashuhudii kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa

kwa haki ila Allah, wanamkidhibisha Mtume (s.a.w.), wanakanusha kufufuliwa Siku ya Qiama na wanaikadhibisha Qur'ani na kuichukulia kama uchawi; nasi twashuhudia na twakiri kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, twaisadiki Qur'ani, twaamini Qiama, twasali na twafunga Ramadhani, basi mnatufananishaje nao? Jawabu ni: 'Ulamaa wote wamekubaliana kuwa mwenye kumsadiki Mtume (s.a.w.) katika jambo lakini akamkadhibisha katika lengine basi huyo ni kafiri wala hajaingia katika Uislamu, na pia akiamini sehemu ya Qur'ani na kuikanusha baadhi yake—huyo mfano wake ni kama aliyekiri Tawhidi na Salah lakini akakanusha ulazima wa Zaka; au akayakiri haya yote ila akakanusha Sawm, au akayakiri haya yote bali akakanusha Hijja. Na ilipotokea kutolaumiwa baadhi ya watu juu ya Hijja zama za Mtume (s.a.w.), kukhusu hilo Allah aliteremsha kauli Yake:

﴿وَلِلهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ البيت من استطاع إليه سبيلا ومن كفر فإنَّ الله غنيٌّ عن العالمين﴾ [سورة آل عمران، الآية: ٩٧].

*Na Allah amewawajibishia watu wafanye Hijja katika Nyumba hiyo; yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha (asiende, na hali ya kuwa anaweza) basi Allah si mhitaji kuwahitajia walimwengu.* (3:97)

Na atakayekiri haya yote na akakanusha kufufuliwa, huyo ni kafiri kwa ijma'i, na ni halali damu na mali yake, kama asemavyo Allah:

قال تعالى: ﴿إنَّ الذين يكفرون بالله ورُسُله ويريدون أن يفرّقوا بين الله ورسله ويقولون نؤمن ببعض ونكفر ببعض ويريدون أن يتخذوا بين ذلك سبيلا أولئك هم الكافرون حقّا﴾(١) الآية

*Hakika wale wanaomkanusha Allah na Mitume Yake, na wanataka kutenga baina ya Allah na Mitume Yake, kwa kusema: "Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa," na wanataka kushika njia iliyo kati ya haya (si ya Kiislamu khasa wala ya kikafiri). Hao ndio makafiri kweli.* (4:150-151)

Basi ikiwa Allah amebainisha waziwazi katika Kitabu Chake kuwa mwenye kuamini baadhi na akakanusha baadhi huyo ni kafiri kweli, mushkili huu utakuwa umetatuliwa na hili ndilo alilolitaja mmoja wa wakazi wa Al-Ihsa', Saudi Arabia katika kitabu chake alichotutumia.

Na pia husemwa: Ikiwa unakiri kuwa mwenye kumsadiki Mtume (s.a.w.) katika kila kitu lakini akakanusha uwajibu wa Salah, basi yeye ni kafiri kwa ijma'i na damu na mali yake ni halali. Hivyo hivyo akikiri kila kitu isipokuwa kufufuliwa; na vile vile lau akanusha uwajibu wa Sawm ya Ramadhani lakini akayakiri mengine yote—madhehebu yote hayakhitilafiani, na Qur'ani imeshalitaja hilo, kama tulivyotangulia kusema hapo awali.

Basi imejulikana kuwa Tawhidi ndio faradhi kuu alokuja nayo Mtume (s.a.w.), nayo ni adhimu kuliko Salah, Zaka, Sawm na Hijja. Sasa itakuwaje mtu awe amekufuru atakapokanusha moja ya nguzo hizi za kimatendo hata ikiwa

anayatekeleza mengine yote alokuja nayo Mtume (s.a.w.); na asikufuru akikanusha Tawhidi ambayo ndio msingi wa Dini ya Mitume wote (a.s.)? Subhanallah! Ujinga ulioje!

Na pia husemwa: Masahaba wa Mtume (s.a.w.) walipigana vita dhidi ya Bani Hanifah[1], na hali walisilimu kwa Mtume (s.a.w.) mwenyewe, nao walikuwa wanakiri Shahada mbili, wanaadhini na kusali. Akisema: Sababu wao walidai kuwa ati Musailamah naye alikuwa Mtume. Tutasema: Hiyo ni kweli. Lakini kumnyanyua mtu hadi daraja ya Utume ni kufuru ambayo huihalalisha damu na mali ya mtu bila ya kumfaa Shahada mbili zake wala Salah; basi je, atakayewapa uungu Shamsani au Yusuf[2] au Sahaba au Nabii? Ametukukuka Mola wa mbingu na ardhi. Ni 'adhimu mno Shani Yake!

سبحانه ما أعظم شأنه! ﴿كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللهُ عَلَى قُلُوبِ الَّذِينَ
لَا يَعْلَمُونَ﴾ [سورة الروم، الآية: ٥٩].

*Hivyo ndivyo Allah anavyopiga muhuri katika nyoyo za wale wasiofahamu.* (30:59)

---

1. Nao ni Musailamah Al-Kadhdhab na wafuasi wake, na Masahaba hawakukhitilafiana katika jambo la kuwapiga vita bali waliwafikiana.

2. Yusuf, Shamsan na Taj ni majina ya baadhi ya wanaotakidiwa katika nchi hiyo, kama vile Badawy, Dusuqy na Al-Mutabawally na kama hao huko Misri; na kama Ibn 'Araby huko Damascus—hayo ameyasema Muhibbudin Al-Khatib. Mungu amrehemu.

Na husemwa pia: Wale alowaunguza 'Aly bin Abi Talib[1] (r.a.) kwa moto, nao wote walijidai Uislamu nao pia walikuwa katika watu wake 'Aly (r.a.) na walipata elimu ya Dini kutoka kwa Masahaba (r.a.) ila waliitakidi kuwa 'Aly (r.a.) ni Mungu kama wanavyoitakidiwa akina Yusuf na Shamsan na mifano yao; na Masahaba waliwafikiana kuwaua na kuwakufurisha. Je, mnadhani kuwa Masahaba waweza kuwakufurisha Waislamu? Je, mnadhani kuwa kuwafanya miungu akina Taj na walio kama yeye haidhuru, lakini itikadi hiyo hiyo kwa 'Aly bin Abi Talib ni kufuru?

Na husemwa vile vile: Bani 'Ubaid Al-Qaddah[2] ambao walitawala Morocco na Misri katika zama za Bani Al-'Abbas, nao wote walishuhudia kwa Shahada mbili wakajidai Uislamu na kusali Salah ya Ijumaa na Salah za jamaa. Lakini pale walipodhihirisha kuikhalifu kwao Shari'ah ya Kiislamu katika baadhi ya mambo kuliko vile tuichukuliavyo sisi kwa ukamilifu wake; ijma'i ya''Ullma wa Kiislamu ilitangaza ukafiri wao na wakawatangazia vita; na kwamba nchi zao ni *Biladu Harb,* basi Waislamu wakawapiga vita mpaka wakazikomboa nchi za Waislamu zilizokuwamo mikononi mwao.

---

[1]Hadith ya kuwa 'Aly aliwaunguza Rafidhah kwa moto, ameitaja Al-Hafidh katika *Fat-hul Bary* 12/282 katika kuisherehesha hadithi ya 'Ikrimah, nambari 6922, 3017.

[2]Hao ndio waliojiita Al-Fatimiyyin kwa hila na uongo tu; nao kama alivyowataja zaidi ya mmoja miongoni mwa 'Ulama: "Dhahiri yao ni Ushia na batini yao ni ukafiri khalisi." Akasema Shaikhul-Islam, Ibn Taimiyyah, "Kubwa wanalolifanyia majidai ni kwamba wao walikuwa wakijidhihirisha kwa Uislamu na kushikamana na Shari'ah zake, lakini si kila mwenye kujihidhirisha kwa Uislamu ni Mu'min katika batini (siri) yake, haya ni kwa sababu wameshatambulikana baadhi ya waliojidhihirisha kwa Uislamu kuwa wengine ni wanafiki; na Allah amesema:

قال الله تعالى: ﴿ومن النّاس من يقول آمنا بالله وباليوم الآخر وما هم بمؤمنين﴾

*Na katika watu, wako (wanafiki) wasemao 'Tumemwamini Allah na Siku ya Mwisho'; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini.* (2:8)

Na hawa walojiita Al-Fatimiyyin wameshuhudiwa na 'Ulamaa wa Umma wa Kiislamu na maimamu wake na makundi yote kuwa wao walikuwa wanafiki wazandiki: wajidhihirisha kwa Uislamu na kuficha kufuru yao.

Basi mwenye kuwashuhudia kwa Uislamu, anawashuhudilia kwa aso na elimu nalo kwa vile hamna kiashiriacho Uislamu wao kinyume ya zile ishara zionyezasho unafiki na uzandiki wao. Pia nasaba yao. Imefahamika kuwa kongamano la Umma wa Kiislamu unashuku nasaba yao na inasemwa kuwa wao ni kizazi cha Mujusi au Wayahudi. (Angalia Majmu' Al-Fatawa 127/35)

Na pia husemwa: Ikiwa watu wa awali hawakukufirishwa ila kwa vile wao walikusanya baina ya shirki na kumkidhibisha Mtume (s.a.w.) au kuikidhibisha Qur'ani au kuikanusha Qiama na kama hayo. Hapa twajiuliza nini maana ya mlango walioutaja 'Ulama katika madhehebu zote kama: "Mlango wa Hukumu ya Murtadi", naye ni Muislamu anayekufurishwa baada ya Uislamu. Kisha wakataja aina nyingi ambazo kila mojawapo humkufurisha mtu na kuihalalisha damu na mali yake, hadi wakataja mambo yaonekanayo ni madogo madogo kwa ayatendayo, kama vile neno alitajalo kwa ulimi wake bila kutoka moyoni khasa, au neno alisemalo kwa njia ya mzaha na mchezo.
Pia husemwa: Wale ambao Allah amewasema:

*Wanaapa kwa (Jina la) Allah (ya kwamba) hawakusema, hali kuwa wamekwishasema neno la ukafiri, na wakakufuru baada ya (kudhihirisha) Uislamu wao (wa uongo).* (9:74)

Je, hujasikia kuwa Allah amewakufurisha kwa sababu ya kutamka neno tu juu ya kuwa walikuwa katika zama za Mtume (s.a.w.), wakienda katika Jihad pamoja naye, wakisali pamoja naye na kutoa Zaka na kuhiji na kuitajataja Tawhidi?

Pia wale alowaambia Allah:

**قال الله فيهم: ﴿قل أبالله وآياته ورسوله كنتم تستهزئون لا تعتذروا قد كفرتم بعد إيمانكم﴾** [سورة التوبة، الأيتان: ٦٥، ٦٦].

*Sema: 'Mlikuwa mkimfanyia mzaha Allah na Aya Zake na Mtume Wake?' Msitoe udhuru (wa uongo); umekwisha kudhihiri ukafiri wenu (mliokuwa mkiuficha) baada ya kule kuamini kwenu (kwa uwongo).* (9:65-66)

Basi hao ndio alobainisha Allah kuwa wamekufuru baada ya Uislamu wao, nao walikuwa pamoja na Mtume (s.a.w.) katika Vita vya Tabuk walitamka jambo ambalo wasema kuwa walilitamka kwa mzaha[1]; hapa angalia kuchanganyikiwa kwa hawa wasemao: "Nyinyi mnawakufurisha miongoni mwa Waislamu watu ambao wametoa Shahada mbili wanasali na wanafunga?" Kisha zingatia jawabu lake, kwani jawabu hilo ndilo lenye faida kubwa zaidi katika nyaraka hizi, na

1. Hadithi hii ameinakili Ibn Jarir At-Tabary kwa isnadi sahihi, kama alivyosema Mahmud Shakir, na nambari yake ni: 16912/14/333.

miongoni mwa dalili juu ya hilo pia ni yale alotusimulia Allah kukhusu Bani Israil pamoja na Uislamu wao, ilimu yao na utengamano wao; pamoja na hayo yote walimwambia Musa (a.s.):

﴿اجعل لنا إلهًا كما لهم آلهة﴾

*Wakasema: 'Ewe Musa! Tufanyie waungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu.'* (7:138)

Na kauli ya watu miongoni mwa Masahaba: "Tufanyie Dhatu Anwat." Hapo Mtume (s.a.w.) aliapa kuwa hii ni kama kauli ya Wayahudi kwa Musa (a.s.): "Tufanyie nasi waungu."[2]

Lakini washirikina wana hali ya kuchanganyikiwa ambayo huidhihirisha katika kisa hiki, kwani husema: "Hao Bani Israil hawakukufuru kwa tamko lao hilo, na kadhalika wale waliomwambia Mtume (s.a.w.): 'Tufanyie nasi *'Dhatu Anwat,'* hawakukufuru?" Jawabu lao ni: Hao Bani Israil hawakulitekeleza hilo tamko lao kimatendo na pia wale walomwambia Mtume (s.a.w.) hawakutekeleza matamshi yao kimatendo. Na hakuna khilafu kuwa lau Bani Israil wangeyatekeleza matamshi yao kimatendo wangekufuru, na pia wale alowazuia Mtume (s.a.w.), lau wasingemtii na wangejifanyia *'Dhatu Anwat'* baada ya kuzuiwa na Mtume (s.a.w.) nao wangekuwa wamekufuru; na hii ndio hakika ya mambo. Lakini kisa hiki chatukumbusha kuwa Muislamu—bali ulimwengu mzima—huenda ukajitumbukiza katika shirki bila ya kutambua, basi hapa tunastafidi kuwa budi kujifunza na kujihadhari, na tujue kuwa maneno ya mjinga: "Tawhidi tumeifahamu", ni ujinga mkubwa na ni miongoni mwa hila za shetani. Na kisa hichi pia chatupa faida nyengine, kuwa Muislamu *mujtahid* akisema

---

2. Hadithi imenakiliwa na Tirmidhi katika Mlango: "Mtazifuata Nyenendo za Waliokuwa kabla Yenu."

Na hadithi hii amesema kuwa ni sahihi Al-'Allamah Al-Albany katika: *Fy Dhilalil-Jannah,* akasema tena kuwa ni sahihi katika kuihariri *Mishkat,* nambari (5408), na Sahih al-Jami' (3601)

Nayo ni kuwa Mtume (s.a.w.) alipotoka kuelekea Humain alipita pahali penye mti wa washirikina uitwao *'Dhatu Anwat'*. Walikuwa wakitundika silaha zao kwenye mti huo. Masahaba wakamwambia Mtume (s.a.w.) tufanyie nasi *'Dhatu Anwat'* kama wao walivyo na *'Dhatu Anwat'*. Mtume (s.a.w.) akasema: "Ametukuka Allah! Haya ni kama yale waliyosema watu wa Musa: 'Tufanyie waungu na sisi kama wao walivyo na miungu'. Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkono Mwake! Mtaufuata mwenendo wa waliokuwa kabla yenu."

maneno ya kufuru bila kujua kisha akazinduliwa, naye akatubu papo hapo, basi huyo hajakufuru. Na hayo ndio waliyofanya Bani Israil na wale Masahaba waliomwomba Mtume (s.a.w.). Faida nyingine ni kwamba japokuwa Muislamu hakufuru kwa jambo kama hilo, anastahiki kukemewa vikali sana kama alivyofanya Mtume (s.a w.).

Nao wana kuchanganyikiwa kwengine, wanasema: "Mtume (s.a.w.) hakuridhishwa na kitendo cha Usamah (r.a.) cha kumuua yule aliyesema: *La ilaha illal-Lah* na akamwambia: 'Je, umemuua baada ya kuwa amesema: *La ilaha illal-Lah?'*"[1]

Na kadhalika kauli yake (s.a.w.): "Nimeamrishwa nipigane na watu mpaka wakubali kuwa hakuna Mola isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah..."[2]

Na ziko hadithi nyengine ambazo kwazo Mtume (s.a.w.) ameamrisha kutomuua ambaye amekiri Shahada mbili.

---

1. Hadithi hii iko katika Fat-hul Bary, 'Kitab-al-Maghazi' nambari 4269 Juz 7/590, na 'Kitab Ad-Diyat' nambari 6872 Juz. 12/119. Na katika Mukhtasar Sahih Muslim cha Al-Mundhiry kilichorejelewa na Al-Abany, Mlango: Atakayeua mtu miongoni mwa makafiri baada ya kuwa amesema: *La ilaha illal-Lah.* Na Al-Mishkat, nambari 3450, na Zadul-Ma'ad cha Ibn Al-Qayyim, Juz. 3 uk. 361 kilichorejelewa na Al-Arnaut. Amesimulia Usamah (r.a.): "Alitutuma Mtume (s.a.w.) katika kikosi cha jeshi huko Al-Harqah, basi tukawashambulia maadui alifajiri na tukawashinda. Nami pamoja na mtu mmoja miongoni mwa Ansari tulipambana na adui mmoja tulipomshinda alisema: *'La ilaha illal-Lah'*, yule Ansari akaacha kumshambulia, lakini mimi nilimchoma kwa mkuki wangu mpaka nikamuua. Tuliporudi kwa Mtume (s.a.w.) aliipata khabari hiyo naye akaniambia: 'Ewe Usamah, ulimuua baada ya kuwa amesema: *'La ilaha illal-Lah?'*

Nikasema: 'Alikuwa akijikinga tu'. Lakini Mtume (s.a.w.) aliendelea kulikariri neno hilo hadi nikatamani ningekuwa sijasilimu kabla ya siku hiyo."

2. Hii ni hadithi *Mutawatir.* Imenakiliwa na Bukhary, nambari 1399; 'Kitabuz-Zakah' 3/300. Na *Fat-hul Bary, 'Babul-I'tisamu Bil-Kitabi was-Sunnah'*, Juz. 13/264. Na *Mukhtasar Sahih Muslim*, cha Al-Mundhiry nambari 4. Na *Musnad Abi Bakr As-Siddiq* cha Abu Bakr Al-Mazuzy nambari 77 na 140. Na Sahih Sunan Ibn Majah, nambari 59 kutoka kwa Abu Hurairah (r.a.) na nambari 60; kutoka kwa Mu'adh bin Jabal (r.a.). Na Sahih Sunan An-Nasai, 'Kitab Tahrim ad-Dam' na Bab Hurmatu Iraqati Dam al-Muslim Bighairi Haq', n.,k. Na lafdhi ya Bukhari: Amesimulia Abu Hurairah: Alipofariki Mtume (s.a.w.) na kutawala Abu Bakr (r.a.), wakakufuru walokufuru miongoni mwa Waarabu, alisema 'Umar (r.a.): "Tutapingana vipi na watu hawa na hali Mtume (s.a.w.) amesema: 'Nimeamrishwa nipigane na watu mpaka wakubali kuwa hakuna Mola isipokuwa Allah, wakifanya hivyo zitahifadhika damu zao na mali zao ila kwa haki ya Uislamu na hesabu yao iko kwa Allah."

Na muradi wa hawa majahili ni kwamba yeyote atmkaye Shahada hakufuru wala hauawi hata akitenda jambo gani. Basi watu kama hao waambiwe: Twajua kuwa Mtume (s.a.w.) aliwapiga vita Wayahudi na kuwateka na hali wakisema: Hapana Mola ila Allah[1] na Masahaba wa Mtume (s.a.w.) waliwapiga vita Bani Hanifah hali wanashuhudia: *La ilaha illal-Lah.* Muhammadun Rasulullah, wanasali na kujidaia Uislamu. Na pia wale alowaunguza moto 'Aliy bin Abi Talib (r.a.).

Na hao majahili wanakiri kuwa anayekanusha kufufuliwa, huyo ni kafiri na halali kuuawa hata kama asema: *La ilaha ilal-Lah.* Na kwamba mwenye kukanusha nguzo yoyote ya Uislamu hukufuru, naye huuawa hata ikiwa ametamka Shahada. Basi itakuwaje isimfae anapokanusha moja ya matawi (furu') na imfae atakapoikanusha Tawhidi ambayo ndio msingi na kichwa cha Dini ya Mtume wote? Lakini hao maadui wa Allah hawakufahamu maana ya zile hadithi. Ama hadithi ya Usamah (r.a.) ni kwamba alimuua mtu ambaye alidai Uislamu kwa sababu ya kudhani kuwa huyo hakudai Uislamu ila kwa kukhofia damu na mali yake. Na mtu adhihirishapo Uislamu inawajibika kutomshambulia mpaka litakapobainika kwake lenye kukhalifu kuwa kwake Muislamu[2].

---

1. Hadithi ya kuuawa Wayahudi wa Bani Quraidhah na kutekwa wake zao na watoto wao, ameinakili Imamul-Bukhari; angalia Fat-hul-Bary, 'Kitabul-Maghazy', nambari 4122 Juz. 7/ 475. Na ameinakili Imam Muslim katika: 'Bab: Al-Hukm Fyman Haraba wa Naqadhal-'Ahd'. Angalia: Mukhtasar Sahihi Muslim, cha Al-Mundhiry, hadithi nambari 1154. Pia ameinakili Al-Hafidh Ibn al-Qayyim katika Zadul-Ma'ad 3/129 kilichorejelewa na al-Arnaut: Amesimulia 'Aisha (r.a.): 'Sa'd alijeruhiwa siku ya Vita vya Khandaq kwa kutupiwa mshale wa mmoja wa Maquraish aitwaye Habban bin al-'Irqah.

Basi Mtume (s.a.w.) akamfanyia hema msikitini ili aweze kumzuru kutoka mahali karibu. Aliporudi Mtume (s.a.w.) kutoka katika Vita vya Khandaq akaweka chini silaha na akaoga, akamjia Jibril (a.s.) na hali apangusa mavumbi kichwani, akamwabia: 'Wewe umeshaweka chini silaha lakini hutaziweka chini wakati huu, nenda uwatokee (maadui). Mtume (s.a.w.) akauliza: 'Wapi?' Akaashiria upande wa Bani Quraidhah. Akawaendea Mtume (s.a.w.), nao wakaikubali hukumu yake, lakini yeye akamwomba Sa'd atoe hukumu. Sa'd (r.a.) akasema: 'Hukumu yangu kwao ni kuwa wauawe wapiganaji wote, watekwe wake na watoto wao na zigawiwe mali zao..."

2 Fahamu ndugu yangu, na Allah akupe sa'ada kwa nuru ya Tawhidi na Akuepushe na balaa za shirki, kwamba ni wajibu kutomshambulia adhihirishaye Uislamu, na kutomtuhumu kwa kufuru na kama hayo mpaka libainike kwake jambo linalokhalifu Uislamu. Na yanayotengua Uislamu yanajitegemeza juu ya kaida kumi miongoni mwa hizo zaingia sura na tafsili nyingi ambazo si sahali kuzihesabu. Hapa twataja kwa mukhtsari mfupi sana: (1) Shirki katika ibada ya Allah. (2) Mwenye kujifanyia wasita baina yake na Allah ambao huwataka uombezi na kuwategemea, kwa

Na Allah (s.w.) ameteremsha kukhusu hilo:

﴿يا أيها الذين آمنوا إذا ضربتم في سبيل الله فتبينوا﴾ [سورة النساء، الآية: ٩٤].

*Enyi Mlioamini! Mtakaposafiri katika Njia ya Allah, basi msifanye jambo ila kwa ithibati..."* (4:94)

Yaani mthibitishe kwanza. Aya hii basi ni dalili kuwa ni wajibu kutomshambulia mwenye kudhihirisha Uislamu na pia kuwa na ithibati. Basi likidhihiri kwake linalokhalifu Uislamu atauawa kwa mujibu wa kauli Yake (s.w.):

﴿فتبينوا﴾

*Basi msifanye jambo ila kwa ithibati...* (4:94)

Na lau ingekuwa hauawi akishatamka Shahada, basi hili jambo la ithibati lisingekuwa na maana. Na kadhalika ile hadithi nyengine na zengine mfano wa hiyo zaashiria yale tuliyoyataja kwamba anayedhihirisha Uislamu na Tawhidi twawajibika kujizuia tusimdhuru ila pale litakapobainika kwake litengualo Uislamu wake, na dalili ya haya ni Mtume (s.a.w.) ambaye alisema: "Je, umemuua baada yakuwa amesoma: *La ilaha ilal-Lah?* Naye pia aliyesema: "Nimeamrishwa nipigane na watu mpaka watakapokubali kuwa hapana Mola ila Allah." Na yeye pia ndiye aliyesema kukhusu Khawarij: "Popote mtakapokutana nao piganeni nao; nami nikidiriki (kukutana nao) nitapigana nao pigano kama la kuwamaliza kina'Adi[1]

---

Ijma'i huyo amekufuru. (3) Ambaye hawakufurishi washirikina au ashuku kuwa hao ni makafiri au aona kuwa madhehebu yao ni sahihi, huyo amekufuru. (4) Mwenye kuitakidi kuwa uongozi mwengine usiokuwa wa Mtume (s.a.w.) ni mkamilifu zaidi, au hukumu nyengine isiyokuwa ya Mtume (s.a.w.) hata kama akitekeleza, huyo ni kafiri. (6) Mwenye kukifanyia istighzai kitu katika Dini ya Mtume (s.a.w.), au thawabu au iqabu yake, huyo amekufuru. (7) Uchawi. (8) Kuwasaidia washirikina dhidi ya Waislamu. (9) Mwenye kuitakidi kuwa baadhi ya watu wanaruhusiwa kujivua na Shari'a ya Mtume (s.a.w.), huyo ni kafiri. (10) Kuitupa na kujitenga na Dini ya Allah si jambo la kujifunza wala kulitenda. Angalia Risalah yangu; 'Ashra Rasali Fit-Tawhidi wan-Najat minash-shirk.

1 Ameinakili Bukhari, angalia Fat-hul-Bary, nambari: 6930 na 6931, 'Babu Istitaabatul-Murtaddin wal-Mu'anidin wa Qitaluhum." Na Nasai 3823 katika As-Sahih cha Al-Albany. Na Sahih Ibn Majah, nambari 138 mpaka 145, na Al-Baghwy katika Sharhus-Sunnah 10/224, na Ibn 'Asim katika Kitabus-Sunnah, Bab: 'Al-Mariqah wa-Hururiyyah wal Khawarij As-Sabiqu laha khudhlanu

Mtume (s.a.w.) amesema hayo kukhusu Khawarij juu ya kuwa wao ni wenye ibada na Tahlili zaidi kuliko watu wengine.

Mambo yalifikia hadi ya kuwa Masahaba walikuwa hawazithamini Salah wanazozisali na hao Khawarij, juu yakuwa wao walijifunza elimu kutoka kwa Masahaba (r.a.). Basi haikuwafaa *La ilaha illal-Lah* wala wingi wa ibada na kujidaia kwao Uislamu pale ilipodhihiri kwao kukhalifu Shari'ah ya Kiislamu. Pia yale tuliyotaja kukhusu kuwapiga vita Wayahudi, na vita vya Masahaba dhidi ya Bani Hanifah, na pia Mtume (s.a.w.) alitaka kuwapiga vita Bani Al-Mustalaq pale mtu mmoja alipomwambia kuwa wamezuia kulipa Zaka mpaka pale alipoteremsha Allah:

﴿يا أيّها الذين آمنوا إن جاءكم فاسق بنبأ فتبينوا أن تصيبوا قومًا بجهالة فتصبحوا على ما فعلتم نادمين﴾ [سورة الحجرات، الآية: ٦].

*Enyi mliominii Fasiki akikujieni na khabari yoyote ile msimkubali (tu) bali pelelezeni (kwanza) msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.* (49:6)

Na hakika ya mambo ni kwamba mtu huyo alikuwa ni mrongo .

---

Khaliqiha', nambari: 910 na 914 mpaka mwisho wa Mlango huo. Hii ni Takhrij Sheikh Al-Albany. Na lafdhi ni ya Al-Bukhari katika hadithi ya 'Aly (r.a.): "...Watatokea watu akhiruz-zaman vijana mabarobaro, wenye ndoto za kisafihi wanazungumza baadhi za kauli za Mtume (s.a.w.) na imani zao hazizami chini zaidi ya viwango vya koo zao, hutoka katika Dini kama utokavyo mshale katika upinde, basi popote mkutanapo nao waueni."

1. Hadithi ameinakili Al-Haithamy katika Majma' Az-Zawaid 7/109 na kusema: Ameinakili Ahmad na Tabarany na wasimulizi wa Ahmad ni wa kutegemewa. Pia ameinakili Ibn Kathir katika Tafsiri yake 4/223. Na Ibn al-Qayyim katika tafsiri yake iitwayo, At-Tafsiri-al-Qayyim, uk. 440. Na lafdhi ya Ibn athir katika hadithi ya Al-Harith bin Dhirar (r.a.): "Nilikuja kwa Mtume (s.a.w.) akanilingania Uislamu nami nikaukubali Uislamu na kuukiri. Kisha akanilingania Zaka nikaikiri na kumwambia: 'Ewe Mtume wa Allah, mimi mitarudi kwao (watu wangu) na nitawalingania Uislamu pamoja na kuwataka kulipa Zaka, basi atakayenikubalia nitakusanaya Zaka yake, nawe unitumie mjumbe katika wakati kadha ili akuletee hiyo Zaka nitakayoikusanya'." Basi alipokusanya Al-Harith Zaka ya wale waliokubali na ukawadia ule wakati aliomtaka Mtume (s.a.w.) amtumie mjumbe, Mtume (s.a.w.) alijizuia kumtuma huyo mjumbe. Basi Al-Harith

Basi haya yote yanathibitisha kuwa muradi wa Mtume (s.a.w.) katika hadithi walizozifanya kuwa ni hoja zao ni muradi ule ule tulioutaja sisi.

Nao wana kuchanganyikiwa kwengine, nako ni kule alikokutaja Mtume (s.a.w.) kwamba watu Siku ya Qiyama watastaghithi kwa Adam (a.s.). Kisha Nuh (a.s.), kisha Ibrahim (a.s.), kisha Musa (a.s.) na 'Isa (a.s.) nao wote watatoa nyudhuru, hadi mwishoni wafike kwa Mtume (s.a.w.). Basi wao husema kuwa jambo hili ni dalili kuwa kustaghithi kwa asiyekuwa Allah si shirki. Na kulijibu hilo twasema: Ametukuka Allah aliyezipiga muhuri nyoyo za maadui Zake! Kustaghithi kwa kiumbe kwa kadri alivyojaaliwa na Allah sisi hatulikanushi jambo hilo—kama alivyosema Allah katika kisa cha Musa (a.s.):

﴿فاستغاثه الذي من شيعته على الّذي مِن عدوِّه﴾ [سورة القصص، الآية: ١٥].

*Basi yule jamaa yake alimowmba msaada dhidi ya yule adui yake.* (28:15)

Na pia anavyostaghithi (anavyoomba msaada) mtu kwa rafiki yake katika vita na mengine miongoni mwa mambo anayoyaweza kiumbe. Sisi tukikanushacho ni kustaghithi kiibada wanakokufanya katika makaburi ya mawalii au katika hali ya kutokuwepo kwao, katika mambo ambayo hayawezi ila Allah[1].

Likikubalika hilo, basi kule kustaghithi watu kwa Manabii Siku ya Qiyama

---

akadhania kuwa ameghadhibikiwa na Allah na Mtume Wake, akawaita wakuu wa watu wake akawaambia: "Hakika Mtume (s.a.w.) alikuwa amenipangia wakati wa kunitumia mjumbe wake ili achukue hii Zaka niliyoikusanya, Mtume (s.a.w.) hakhalifu ahadi yake, nami sioni sababu ya kumzuia mjumbe wake kuja kwetu ila kwa sababu ya ghadhabu (aliyotughadhibikia) basi twendeni kwa Mtume (s.a.w.)'. Lakini Mtume (s.a.w.) alikuwa ameshamtuma Al-Walid bin 'Uqbah kwa Al-Harith ili akaichukue Zaka alokuwa nayo. Alipofika huko mbali akaogopa kuendelea, basi akarudi kwa Mtume (s.a.w.) na kumwambia: 'Ewe Mtume wa Allah! Hakika Al-Harith amenizuilia Zaka na akataka kuniua.' Akaghadhibika Mtume (s.a.w.) akatuma ujumbe kwa Al-Harith (r.a.). Naye Al-Harith akaja na watu wake na kukutana na ujume wa Mtume (s.a.w.) nje ya Madina, naye akawauliza: 'Mmetumwa kwa nani?' Wakasema: 'Kwako.' Akasema: 'Kwa nini?' Wakasema: 'Mtume (s.a.w.) alikutumia Al-Walid bin 'Uqbah, naye amedai kuwa wewe umemzuilia Zaka ukataka kumuua.' Akasema (r.a.): 'La! Naapa kwa Yule aliyemtuma Muhammad (s.a.w.) kwa haki. Mimi sikumwona kabisa wala hakunijia. Nami sikuja ila nilipoona hakunifikia mjumbe wa Mtume (s.a.w.); kwani nimekhofia isijekuwa ni ghadhabu ya Allah na Mtume Wake juu yetu.' Akasema: Ikateremka kauli Yake Allah: (49:6).

1 Na hata katika mambo ambayo ayaweza kiumbe haijuzu kustaghithi kwa maiti au asiyekuwapo hapo.

kwamaanisha kutaka msaada wao kwa kumwomba Allah awahasibu watu ili wastarehe walioandikiwa Pepo kutokana na misukosuko ya siku hiyo. Na hili lajuzu duniani na Akhera; kuwa umwendee mtu mwema mcha-Mungu akae akusikilize umwambie: 'Niombee kwa Allah', kama walivyokuwa Masahaba (r.a.) wakimwomba Mtume (s.a.w.) katika uhai wake. Ama baada ya kufariki kwake, hasha kawakumwomba katika kaburi lake, bali wamezuia As-Salaf kumwomba Allah kwenye kaburi la Mtume (s.a.w.), basi kukoje kumwomba yeye mwenyewe (s.a.w.) hali ameshafariki?

Nao wana kuchanganyikiwa kwengine, nako kuko katika kisa cha Nabii Ibrahim (a.s.) pale alipotupwa motoni, akamjia Jibril (a.s.) akiwa juu hewani akamwambia: "Je, una haja yoyote?" Akasema Ibrahim (a.s.): "Ama kwako wewe la (sina haja.)."[1]

Wakasema: Lau kustaghithi (kutaka msaada) kwa Jibril kungekuwa ni shirki, yeye Jibril (a.s.) asingemu'aridhia Ibrahim (a.s.). Jawabu: Huku kunafanana na kule kuchanganyikiwa kwa kwanza, kwani Jibril (a.s.) alimu'aridhia Ibrahim (a.s.) kwa jambo aliwezalo. Na hayo ni kama alivyosema Allah kukhusu Jibril (a.s.):

*Mwenye nguvu sana.* (53:5) ﴿شديد القوى﴾ [سورة النجم، الآية: ٥].

Na lau Allah angemruhusu kuuchukua huo moto wa Ibrahim na ardhi na majabali yaliyozunguka na kuvitupa hivyo vyote mashariki au magharibi angefanya

---

1 Ameitaja Al-Baghwy katika Tafsiri ya Suratul-Anbiya' hali ya kuashiria udhaifu wa hadithi yenyewe; Amesimulia Ka'b al-Ahbar (r.a.) kuwa Ibrahim (a.s.) walipomtupa kwa al-Manjaniq, mashine ya kutupia kitu kwa mbali, alimkabili Jibril (a.s.) ambaye alimwambia: 'Je, una haja yoyote?' Akasema: 'Ama kwako, la (sina haja).' Akasema Jibril (a.s): 'Basi mwombe Mola wako.' Akasema Ibrahim (a.s.): 'Elimu Yake kukhusu hali yangu yatosheleza kuliko kumwomba kwangu.'

Na Ibn Kathir ameinasibisha kwa baadhi ya As-Salaf 3/193.

Amesema Sheikh Al-Albany katika As-Silsilah Adh-Dha'ifah nambari 21 kuwa hii haina asili. kisha akasema: 'Kwa jumla maneno haya aliyopachikwa Ibrahim (a.s.) hayawezi kutamkwa na Muislamu ajuaye umuhimu wa du'a katika Uislamu, basi atayatamkaje Ibrahim (a.s.) aliyetwita Waislamu? Kisha nimeikuta hadithi hii ameitaja Ibn 'Iraq katika: Tanzih ash-Shari'ah al-Marfu'ah 'an al-Akhbar Ash-shani'ah al-Maudhu'ah. Akasema katika 1/250 amesema Ibn Taymiyyah hii ni hadithi maudhui.'

hivyo. Na lau Angemwamrisha ampaishe Ibrahim (a.s.) mbinguni, angempaisha. Na mfano wa haya ni kama mtu tajiri mwenye mali nyingi amwone mtu muhitaji na amwambie kuwa kama apendelea, basi yeye aweza kumkopesha, au kumpa kitu ili atimizie haja zake, lakini huyo mtu muhitaji akatae kuchukua msaada huo, bali asubiri mpaka Allah amletee riziki ambayo hamna mtu atakayeweza kumsemea kwa lolote. Basi hili liko mbàli kiasi gani na istighatha ya ibada na shirki—lau watu hawa wanafahamu?[1]

Na tuyakhitimishe maneno yetu, Insha-Allah—kwa mas'ala muhimu sana, ambayo yafahamika kutokana na yaliyotangulia, lakini hapa twayazungumza kwa urefu kwa sababu ya umuhimu wake mkubwa na kwa vile mas'ala haya hukosewa sana; twasema:

Hakuna khilafu kuwa Tawhidi budi iwe kwa moyo, ulimi na vitendo; likikosekana mojawapo kwa mtu, basi huyo si Muislamu. Akiijua Tawhidi lakini akatae kuitekeleza kimatendo, huyo ni kafiri mwenye inadi kama ya Fir'auni, Ibilisi na kama hao. Na hapa ndipo wakoseapo watu wengi wakisema: "Hii ni kweli, nasi twalijua hilo, lakini hatuwezi kulifanya, na wala halijuzu kufanywa kwa watu wa miji yetu, na mtu awajibika kuwafikiana na watu wa mji wake."

Nao watoa nyudhuru nyingi. Na maskini hao hawajui kuwa wengi wa viongozi wa kufuru huijua haki, nao hawaiachi hiyo haki ila kwa udhuru miongoni mwa nyudhuru zao, kama alivyosema Allah:

﴿اشْتَرَوْا بِآيَاتِ اللهِ ثَمَنًا قَلِيلًا﴾

*Wamekhitari thamani ndogo (ya kidunia) kuliko kufuata Aya za Allah.* (9:9)

Na ziko aya nyingi zengine za Allah kama vile:

---

1 Wale wanaostaghithi kwa makaburi—Allah awaongoze, wanashindwa kutambua—kuwa maiti hawasikii du'a za wawaombao kwa hali yoyote; na hayo ni kwa mujibu wa kauli Yake (s.w.):

لقوله تعالى: ﴿إن تدعوهم لا يسمعوا دعاءكم﴾

*Kama mkiwaomba hawasikii wito wenu...* (35:14)

Nami nawasihi kusoma kitabu cha Al-'Allamah Al-Alusy: *Al-Ayatul Bayinat Fy 'Adami Sima'il Amwat* kilichorejelewa na Shaikh Al-Albany.

﴿يعرفونه كما يعرفون أبناءهم﴾ [سورة الأنعام، الآية: ١٩].

*...Wanayafahamu haya kama wanavyowafahamu watoto wao...* (6:20)

Na akiitekeleza Tawhidi kwa dhahiri naye haifahamu hiyo Tawhidi au haiitakidi kwa moyo wake, basi huyo ni mnafiki, naye ni mbaya zaidi kuliko kafiri khalisi kwa mujibu wa kauli Yake (s.w.):

﴿إنّ المنافقين في الدرْك الأسفل من النّار﴾ [سورة النساء، الآية: ١٤٥].

*Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika Moto.* (4:145)

Na mas'ala haya ni mas'ala makubwa na marefu, nayo yatakubainikia pale utakapoyazingatia yatokapo katika ndimi za watu. Utawakuta watu ambao wanaijua haki lakini hawaitendi kwa kukhofia kupungukiwa mapato yao ya kidunia, au jaha, au kwa kutaka kuwaridhisha wengine. Na kuna wale waitekelezao Tawhidi kwa dhahiri tu mbele za watu, na ukimuuliza kukhusu hicho anachokiitakidi moyoni mwake utamkuta yeye mwenye hakijui. Ni wajibu wako basi kuzifahamu vizuri aya mbili katika Kitabu cha Allah, ya kwanza ni ile liyotangulia:

﴿لا تعتذروا قد كفرتم بعد إيمانكم﴾ [سورة التوبة، الآية: ٦٦].

*Msitoe udhuru (wa uwongo) umekwisha kudhihiri ukafiri wenu (mliokuwa mkiuficha) baada ya kule kuamini kwenu (kwa uwongo).* (9:66)

Na ikisha kukuhakikia kuwa baadhi ya Masahaba ambao pamoja na Mtume (s.a.w.) walifanya vita dhidi ya Warumi walikufuru kwa sababu ya neno walilosema kwa njia ya mzaha na mchezo, hapo itakubainikia kuwa mwenye kuzungumza kwa mambo ya kufuru au kuyatenda kwa kukhofia kupungua mali yake au jaha yake au kwa ajili ya kumridhisha fulani—huyu mwenye kufanya haya ana makosa makubwa zaidi kuliko yule aliyetamka neno kama hilo kwa njia ya mzaha.

Na aya ya pili ni:

والآية الثانية قوله تعالى: ﴿من كفر بالله من بعد إيمانه إلا من أكره وقلبه مطمئن

﴿بالإيمان﴾ [سورة النحل، الآية: ١٠٦].

*Anayemkufuru Allah baada ya Uislamu wake (inamngojea adhabu kubwa) isipokuwa yule aliyeshurutishwa, hali ya kuwa moyo wake umetuwa juu ya Uislamu (wake).* (16:106)

Hapa ni dhahiri kuwa Allah hakukubali ila udhuru wa yule mwenye kushurutishwa na hali moyo wake umetuwa juu ya Uislamu; na mwengine yeyote mwenye kukosa sifa hizo basi huyo amekufuru baada ya kuwa kwake Muislamu, iwe amefanya hayo kwa khofu au kwa ajili ya kumridhisha fulani au kuipendelea nchi yake au familia yake au jamaa zake au mali yake, au amefanya hayo kwa ajili ya mizaha, au kwa lengo lolote lengine—ila awe ameshurutishwa; na hiyo aya yenyewe yaashiria haya haya kwa njia mbili: Kwanza: Kauli ya Allah:

﴿إلا من أكره﴾

*Ila yule mwenye kushurutishwa.*

Twaona hapa Allah hakumvua ila aliyeshurutishwa, na yajulikana kuwa mtu hashurutishwi ila juu ya vitendo au maneno. Ama 'aqida ya moyo basi hakuna anayeshurutishwa kwayo.
Pili: Kauli ya Allah

والثانية قوله تعالى: ﴿ذلك بأنهم استحبّوا الحياة الدّنيا على الآخرة﴾ [سورة النحل، الآية: ١٠٧].

*Hayo (ya kuadhibiwa) ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya dunia kuliko Akhera.* (16:107)

Basi pamebainishwa kuwa huo ukafiri na hiyo adhabu haikuwa kwa sababu ya itikadi au ujinga au kubughudhi Dini au kwa sababu ya kuupenda ukafiri. Lakini sababu yake ya kweli ni kuwa nyuma ya hayo kuna sababu za maslahi ya kidunia, naye ameifadhilisha zaidi dunia kuliko Dini.

Na Allah (s.w.) ndiye Ajuaye zaidi.
Na shukrani zote ni Zake, Mola wa walimwengu. Sala na salamu zimwendee Mtume Muhammad, Aali na Sahaba zake wote.

*Tamati.*

Kwa uwezo wa Allah kilimalizika usiku wa Alkhamisi, Mwezi Ishirini na moja, Dhul-Hijjah 1411H. Sawa na 4/7/1991 C.E.

Mas'ad
Algeria

Amekiandika Abu Anas Al-Husain bin 'Umar Mazuzy

Allah amwonyeshe upole Wake.